**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1328


# Tamathali za Usemi na Uchimuzi wa Maudhui ya Mamlaka katika *Asali Chungu*

**Victor Kyomuhendo, Samuel M. Obuchi & Mosol Kandagor**
*Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-03-22
Kurekebishwa: 2025-09-16
Kukubaliwa: 2025-09-20
Kuchapishwa: 2025-09-24

**Maneno Muhimu**
Mamlaka
Mtindo
Uchimuzi
Ukiushi

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Kyomuhendo, V., Obuchi, S. M., & Kandagor, M. (2025). Tamathali za Usemi na Uchimuzi wa Maudhui ya Mamlaka katika *Asali Chungu*. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(2), 45-54.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Lengo la makala haya ni kuchunguza jinsi Said Ahmed Mohamed anavyotumia tamathali za usemi mbalimbali kama vipengele vya kimtindo katika kuibua maudhui ya mamlaka katika riwaya yake ya *Asali Chungu*. Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi, hasa mhimili wa ukiushi wa nadharia hiyo. Data ilikusanywa kwa kunakili madondoo kutoka katika riwaya ya *Asali Chungu*. Usampulishaji ulifanywa kimaksudi kwa kulenga madondoo yanayochimuza maudhui ya mamlaka katika riwaya hiyo. Uchanganuzi wa data ulifanywa kitaamuli kwa kutambulisha ruwaza na mienendo ya kiisimu iliyobainika katika madondoo. Kisha, uamilifu wa ruwaza na mienendo hiyo ulichanganuliwa kwa kuzingatia muktadha wa ruwaza na mienendo hiyo, mintarafu suala la mamlaka. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba sitiari na kinaya ndizo tamathali za usemi zilizotumiwa hasa na mwandishi kusawiri maudhui ya mamlaka katika riwaya yake. Utafiti huu unapendekeza kwamba uchunguzi kuhusu tamathali za usemi uhusishwe na vipengele vingine vya kimtindo kama vile kipengele cha kileksika na cha kisintaksia.

## Utangulizi

Katika makala haya tunachunguza tamathali za usemi kama kipengele cha mtindo kilichotumika katika kuibua maudhui ya mamlaka katika riwaya ya *Asali Chungu*. Mamlaka ni fenomenoni muhimu ya kijamii kwa sababu inaathiri maisha ya wanajamii. Hata hivyo, uchunguzi wa riwaya hiyo haujaizingatia sana fenomenoni hii. Baadhi ya watafiti walioichunguza riwaya ya *Asali Chungu* ni pamoja na Muriithi (2017) ambaye anaangazia itikadi katika riwaya hiyo, na Osoro (2003) ambaye anahakiki riwaya kadha za Said Ahmed Mohamed, mkiwemo *Asali Chungu*.

Mwandishi anaangazia mahusiano ya kidhalimu na kiunyonyaji kati ya raia wenye nguvu za kiuchumi na raia wasio na nguvu za kiuchumi. Misingi ya mamlaka ya mwenye nguvu ni rasilimali kama vile ardhi na nafasi serikalini, pamoja na mali ambayo ameweza kuipata kutokana na rasilimali hizo. Wakati ambapo mwenye nguvu za kiuchumi anaishi maisha ya starehe, mnyonge anashindwa kuhimili hata gharama ya mahitaji ya msingi ya maisha.

Mbatiah (2001) anaelezea tamathali za usemi kama ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Naye Abrams (1978) anasema kuwa lugha ya kitamathali hukiuka kile ambacho tunakijua kama maana ya kawaida au mfuatano wa kawaida wa maneno ili kuleta maana maalum au athari. Maelezo ya Abrams yanaashiria kwamba tamathali za usemi hukiuka kaida za kiisimu kisemantiki au kisintaksia.

Kipengele cha ukiushi ni cha muhimu sana katika kuzichanganua tamathali za usemi kwa vile ukiushi ndiyo njia anayoitumia mwandishi kusitiri ujumbe wake. Ukiushi unachochea raghba ya msomaji kutaka kujua jambo analolizungumzia mwandishi. Njia mojawapo ya kufikia ujumbe wa mwandishi ni kufasiri matumizi ya tamathali za usemi zilizotumika katika kazi ya kifasihi. Katika fasiri, msomaji anasaidiwa na taswira zilizojengeka katika tamathali za usemi.

Miongoni mwa tamathali za usemi anuwai zilizotumika katika riwaya ya *Asali Chungu*, makala haya yatajikita katika tamathali za usemi chache ambazo zinachimuza maudhui ya mamlaka. Tunachunguza matumizi ya tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, tashihisi na kinaya. Aina hizi za tamathali za usemi zitadhihirishwa katika makala haya kwa madondoo husika kutoka katika riwaya ya *Asali Chungu*.

**Dhana ya Mamlaka**

Kwa mujibu wa TUKI (2013) mamlaka ni "amri au uwezo wa juu wa kuongozea jambo, shirika au shughuli fulani." Nao Thomas na wenzake (2004) wanaeleza kwamba mamlaka ni "uwezo wa wenye mamlaka kuwafanya watu wengine kutii au kufuata ridhaa ya wenye mamlaka hayo." Fasili hizi zinaangalia mamlaka kama uwezo wa mtu wa kuamua au wa kuathiri tabia ya watu wengine.

Dahl (1957) anafafanua kwamba dhana ya mamlaka inafasiliwa kwa mujibu wa mahusiano kati ya watu, na inaelezwa kwa njia ya ishara ambapo mtu A anakuwa na mamlaka juu ya mtu B ikiwa mtu A anaweza kumfanya mtu B atende kitu ambacho mtu B hangetenda. Hivyo, anaeleza kwamba mamlaka yanakuwepo ikiwa kuna mahusiano kati ya watendaji kama vile watu binafsi, makundi, maofisi, serikali na mataifa.

Dahl (1957) pia anaeleza kwamba msingi wa mamlaka ya mtendaji unahusisha rasilimali zote kama vile fursa, vitendo, na vitu ambavyo anaweza kuvitumia ili kuiathiri tabia ya mtu mwingine. Hata hivyo, anaonyesha kuwa mamlaka yanakuwa fiche, yaani hayadhihiriki mpaka yanapotumiwa. Mamlaka yanaweza yakatumiwa kwa njia ya vitisho au kwa msingi wa rasilimali alizo nazo mtu.

Kulingana na Fairclough (1989), fenomena za kijamii, ingawa sio zote, ni za kiisimu kwa vile lugha hutumiwa katika miktadha ya kijamii. Hii inaonyesha kwamba dhana ya mamlaka, ambayo ni fenomenoni ya kijamii, inabainika katika lugha ya kazi za kifasihi. Lugha inayotumiwa na mwandishi mara nyingi huakisi kile kinachoendelea katika jamii. Kwa hivyo, suala la mamlaka linaweza kuchunguzwa kwa kuzingatia lugha iliyotumiwa katika kazi za kifasihi. Katika uchunguzi huu tunaangazia suala hili kwa kuzingatia tamathali za usemi zilizotumiwa katika ya riwaya ya *Asali Chungu*.

**Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi. Kipacha na Jilala (2021), wanatumia istilahi 'mchomozo.' Wanaeleza kwamba mchomozo ni njia ya kukifanya kipengele fulani cha matini kijitokeze zaidi kuliko vipengele vingine. Kwa mujibu wa Peer na Hakemulder (2006) uchimuzi unarejelea mbinu za kiisimu, yaani ukiushi na usambamba, zinazotumika katika matini za kifasihi kwa njia ya kiuamilifu. Mbinu hizi zinaongeza uwezo wa matini wa kujenga maana na wakati huo huo zinaweza kumwathiri msomaji kiujumi.

Nadharia ya Uchimuzi iliasisiwa na wanaisimu wa Tapo la Prague katika karne ya ishirini. Nadharia hii ililenga kuweka uhusiano kati ya viwango vya maumbo ya lugha na maana za matini, jambo ambalo lingemwezesha msomaji kusimbua ujumbe wa mwandishi. Wanaisimu hawa walilenga athari za kisaikolojia za matumizi ya miundo husika ya lugha katika kuielewa kazi ya kifasihi.

Arnold (kama anavyorejelewa na Menialo, 2020) anaamini kwamba uchimuzi unasisitiza vivuli vya maana, na kwa kumfanya msomaji azingatie sehemu fulani za matini, unamsaidia kuona uhusiano kati ya mawazo na umuhimu wa picha mahsusi pamoja na matukio ili aweze kufasiri matini nzima. Mihimili ya Nadharia ya Uchimuzi ni ukiushi na usambamba. Katika uchunguzi huu tunazingatia mhimili wa ukiushi. Kwa mujibu wa Mbatiah (2001), ukiushi ni uvunjaji kimaksudi wa kaida za matumizi ya lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza. Tamathali za usemi zinadhihirisha ukiushi wa kisemantiki. Hivyo, tunachunguza jinsi zilivyotumiwa katika riwaya ya *Asali Chungu* kujenga maudhui ya mamlaka.

**Mbinu za utafiti**

Mbinu za utafiti zilizotumiwa katika uchunguzi huu zilihusisha vipengele vifuatavyo:

**Ukusanyaji wa data**

Ukusanyaji wa data uliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi. Mtafiti aliisoma riwaya ya *Asali Chungu* kwa makini huku akiteua madondoo yenye tamathali za usemi zinazochimuza maudhui ya mamlaka katika riwaya hiyo. Tamathali za usemi ambazo hazikuchimuza maudhui ya mamlaka hazikuzingatiwa. Kwa vile mtafiti aliteua madondoo yanayohusiana na suala mahsusi la mamlaka peke yake, aliweza kuisoma riwaya nzima huku akitafuta madondoo yenye tamathali za usemi husika.

**Usampulishaji**

Katika uchunguzi huu tulitumia usampulishaji lengwa kwa vile tulilenga kuchunguza suala la mamlaka katika riwaya ya *Asali Chungu*, na sio masuala mengine. Hata hivyo, tulizingatia madondoo machache kati ya madondoo yenye tamathali za usemi zinazochimuza maudhui ya mamlaka katika riwaya hiyo. Katika usampulishaji tuliongozwa na Nadharia ya Uchimuzi vilevile. Madondoo yaliyochaguliwa ni yale yaliyovuta udadisi wetu kwa mujibu wa suala la mamlaka.

**Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ya uchunguzi huu ulifanywa kimaelezo. Data ilichanganuliwa kwa kuzitambulisha ruwaza na mahusiano mbalimbali katika data, mintarafu kipengele cha tamathali za usemi na suala la mamlaka. Tulizifafanua tamathali za usemi zilizobainika katika data, halafu tukafasiri uamilifu wa matumizi ya tamathali hizo za usemi katika kuibua maudhui ya mamlaka katika riwaya ya *Asali Chungu*. Katika kufasiri umuhimu na uamilifu wa matumizi ya kila tamathali ya usemi husika, tulizingatia uchimuzi wa maudhui mahsusi ya mamlaka katika dondoo. Fasiri ilifanywa kwa kutumia udadisi, utambuzi, na ubunifu wa mtafiti. Ufahamu unaotokana na mpango wa ulimwengu halisi uliomo akilini mwa mtafiti ulimsaidia kujenga ulimwengu wa kubuniwa wa riwaya ya *Asali Chungu*, mintarafu suala la mamlaka.

**Tamathali za Usemi Zinazochimuza Maudhui ya Mamlaka katika riwaya ya *Asali Chungu***

**Sitiari**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), sitiari ni tamathali ya usemi yenye maana ya kuhusisha kitu kimoja na kingine chenye sifa zinazofanana. Naye Mbatiah (2001) anaeleza kwamba sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi, ambapo vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile vinalinganishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwa kuvilinganisha vitu hivyo, sitiari huonyesha jinsi vitu hivyo vinavyofanana kisifa. Hii inamsaidia msomaji kuelewa kile kinachozungumzwa na mwandishi.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, sitiari kadha zimetumika ili kuibua maudhui ya mamlaka. Sitiari kuu ambayo ndiyo inayojenga maudhui makuu ya riwaya hii ni 'asali chungu.' Msingi wa sitiari hii ni kwamba kiasili asali huwa ni tamu sio chungu. Inabidi msomaji achunguze uamilifu wa

uchimuzi wa kisemantiki ambapo mwandishi ameipa asali sifa ya uchungu. Kazungu (1982) anafafanua kwamba anwani ya maandishi huwa na wajibu wa kutoa fununu kwa msomaji kuhusu ujumbe mkuu au maudhui katika maandishi hayo. Sitiari ya 'asali chungu' imetumiwa na Said Ahmed Mohamed kujenga motifu kwamba mwenye mamlaka, akiyatumia mamlaka hayo vibaya kwa vitendo vya kidhalimu, mwishowe atajutia vitendo hivyo. Mhusika mkuu Zuberi ametumiwa kudhihirisha motifu hii.

1. Jicho lake likaanza kuzunguka. Likamtazama mkewe… halafu likaangalia kivuli cha Semeni… Halafu akamtazama Shemsa; tena… Latifa, na mwisho jicho lake likatua kwa Dude... akameza mate. Yalikuwa mate mazito machungu… Kweli **utamu umegeuka uchungu**… Kama aliwahi kunywa asali, ndipo leo kajua kuwa asali chungu. (*Asali Chungu,* Ukur. 186)

Dondoo la 1 linadhihirisha matokeo ya matumizi mabaya ya mamlaka. Ingawa Zuberi anafurahia uwezo wake wa kumbaka msichana mnyonge Semeni bila kuhofia adhabu yoyote, hatimaye matokeo ya kitendo hiki ni machungu kwake. Hii ndiyo maana ya sitiari "asali chungu," yaani "utamu umegeuka uchungu," kama mwandishi anavyosema. Majuto yake yanatokana na hali kwamba amegundua kwamba Dude ni mtoto aliyetokana na kitendo chake cha kumbaka Semeni. Tena mtoto huyo amekwishahusika kimapenzi na mke wake Zuberi, pamoja na dada zake wa kambo Shemsa na Latifa. Kwa njia hii, mwandishi anaonyesha kwamba mwenye nguvu ameadhibiwa kwa kitendo cha kumwonea myonge.

Asali imerejelewa kisitiari pia kama pesa. Pesa zinampa mtu ushawishi mkubwa. Mbali na kuzitumia pesa kuwashawishi vijana kumstarehesha, Amina anajaribu kuzitumia pesa pia kumshawishi Dude kuacha mpango wa kumwoa Shemsa, bintiye Amina. Anapata ushauri huu kutoka kwa Biti Daudi.

2. **Buyu la asali** umempa mwenyewe ati; unafikiri ampate Shemsa amwache bure bure? *(Asali Chungu,* Ukur. 153)

Katika muktadha wa dondoo la 2, sitiari '**buyu la asali**' inarejelea pesa. Fasiri yetu inatokana na jinsi Biti Daudi anavyomshauri Amina kutumia pesa kumshawishi Dude. Biti Daudi anamkumbusha Amina kwamba hata yeye mwenyewe (Amina) alishazitumia pesa kumshawishi Dude. Pesa ni kama kifaa kinachompa mtu mamlaka ya kushawishi. Kwa maneno ya Bi Mwanakweli (mhusika katika riwaya hii), "ukiwa na pesa una kila kitu" (*Asali Chungu*, Ukur. 107).

Mamlaka kwa njia ya unyonyaji yanadhihirika vilevile katika *Asali Chungu* tukiangalia jinsi ambavyo mwenye uwezo wa kiuchumi (Bi Amina) anavyoutumia uwezo huo kuwaajiri vijana kumfurahisha kimapenzi. Kwa vile vijana hawa hawana uwezo wa kiuchumi ni rahisi kunyonywa na matajiri kama Amina.

3. 'We poa bibiye, usitaharuki. Niachie mie; mambo yote yatakuwa waa, waa kabisa. Nitafuzu kama nilivyofuzu kwa yule kijana msalihina, nikamteka akawa **mali yako**.' (*Asali Chungu*, Ukur. 62)

Katika dondoo la 3 tunaona kwamba mwenye nguvu za kiuchumi (Bi Amina) anawatumia vijana wanyonge kama mali. Katika sitiari 'mali yako' binadamu analinganishwa na mali moja kwa moja kwa sifa ya kumilikiwa. Mwandishi anatumia sitiari ya 'mali yako' kwa sababu anakusudia kuendeleza maudhui ya unyonyaji ambapo mwenye nguvu za kiuchumi anamnyonya asiye na nguvu za kiuchumi.

Said Ahmed Mohamed anaendeleza maudhui ya kutokuwepo usawa wa kiuchumi katika jamii ambapo kuna matabaka ya raia wenye nguvu kubwa za kiuchumi na raia wasio na nguvu hizo, yaani maskini. Mohamed anaendeleza maudhui hayo kupitia kwa sitiari inayorejelea makazi ya watu maskini.

4. Wakapita Ng'ambo ambako majumba, kama kawaida, yalikuwa yamekaliana ovyo, matonge kwa matone… 'kila ndege huruka kwa mbawa zake.' Bali kwa dhahiri, **mbawa za watu wengi huku Ng'ambo zilikuwa dhaifu**.
(*Asali Chungu,* Ukur. 89)

Mwandishi anatumia sitiari '**mbawa za watu wengi huku Ng'ambo zilikuwa dhaifu**' kulinganisha uwezo wa kiuchumi wa wakazi wa eneo la Ng'ambo na mbawa za ndege. Wakazi wameelezwa kama kwamba ni ndege ambao mbawa zao ni dhaifu na hawezi kuruka. Wakazi wa Ng'ambo ni wanyonge kiuchumi. Unyonge huu unaonyeshwa katika maelezo kuhusu nyumba zao duni. Kwa njia isiyo ya moja kwa moja, mwandishi anazilinganua nyumba za raia maskini wa Ng'ambo na nyumba za matajiri, kwa mfano nyumba ya Zuberi, ambayo mwandishi anasema ni kama hoteli.

### *Tashbihi*

Tashbihi ni tamathali nyingine inayotumiwa na Said Ahmed Mohamed kuwasilisha maudhui ya mamlaka katika riwaya yake ya *Asali Chungu*. Wamitila (2003) anaeleza kuwa tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Anasema kwamba tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungio kama vile: 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya', 'ja' na 'kama vile.' Tashbihi vilevile inamwezesha msomaji kujenga taswira fulani akilini mwake wakati akijaribu kuielewa kazi ya kifasihi.

Said Ahmed Mohamed (1978) anaitumia tashbihi pia kusawiri maudhui ya utabaka. Maudhui ya utabaka yanahusiana na suala la mamlaka. Mwandishi anaelezea tofauti kati ya uwezo wa kiuchumi wa tabaka la matajiri kama Zuberi kwa upande mmoja na unyonge wa kiuchumi wa tabaka la raia maskini.

5. Nyumba ilikuwa imeamka. Matayarisho mbalimbali yameshafikia kileleni. **Nyumba hii ilikuwa mfano wa hoteli**; hamkani na shughuli huanza kabla jua halijapasua, na kumalizikia pale bwana na bibi mwenye nyumba wanapoingia chumbani mwao kulala. (*Asali Chungu,* Ukur. 11)

Mwandishi anatumia tashbihi "**nyumba hii ilikuwa mfano wa hoteli**" kuilinganisha nyumba ya Zuberi na hoteli. Tashbihi hii inaonyesha kwamba Zuberi ni mtu wa tabaka la matajiri. Yeye ni ofisa wa serikali mwenye nguvu kubwa za kisiasa na za kiuchumi. Hivyo, ana ushawishi mkubwa katika jamii. Kwa mujibu wa Dahl (1957) msingi wa mamlaka unahusisha rasilimali alizo nazo mtu ambazo anaweza kuzitumia kuathiri tabia za watu wengine. Nyumba ambayo ni mfano wa hoteli ni ishara na pia msingi wa mamlaka aliyo nayo Zuberi.

Mbali na matumizi ya sitiari, mahusiano ya kiunyonyaji kati ya mwenye nguvu za kiuchumi na mnyonge yameelezwa vilevile kupitia kwa tashbihi. Katika mahusiano haya, mnyonge anayenyonywa na mwenye nguvu anashindwa kuzuia unyonyaji huo. Kwa mfano, Amina anatumia uwezo wake mkubwa wa kifedha kuwaajiri vijana kumstarehesha kimapenzi. Lakini anatumia mamlaka yake kuwafukuza anapotaka.

6. Alimwepuka [Dude] makusudi… Dude sasa ni kiraha; kinyaa… Moyo wake ulikuwa umeshaamua… **Atamtema Dude kama mate**… (*Asali Chungu,* Kur. 128 – 129)

Tashbihi '**atamtema kama mate**' inaashiria uamuzi wa Amina usiobadilika na tena mahusiano ya kimamlaka kati ya mwenye nguvu na mnyonge. Anayetema (Bi Amina) ndiye mwenye nguvu za kiuchumi. Naye anayetemwa (Dude) ndiye mnyonge. Dude analinganishwa na mate yaliyotemwa, baada ya kuachwa na mwenye nguvu za kiuchumi. Baada ya kutemwa vijana wanakosa ufadhili kutoka kwa tajiri. Wanarudi kwenye hali ya unyonge wa kiuchumi, bila rasilimali yoyote.

***Tashihisi***

Mbali na sitiari na tashbihi, mwandishi wa *Asali Chungu* amesawiri maudhui ya mamlaka kwa kutumia mbinu ya tashihisi. Wamitila (2003) anaielezea tashihisi kama tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna ilivyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Anasema tashihisi aghalabu pia hurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za kibinadamu. Naye Mbatiah (2001) anafafanua kuwa mbali na kuvihusisha vitu vya kimaumbile kama vile miti, milima na mito, tashihisi pia inatumiwa kuvipa uthabiti vitu dhahania kwa njia ya sifa za kibinadamu. Anafafanua kwamba kitu kinapopewa uthabiti kwa njia hii, huwa kinaeleweka vizuri zaidi.

Said Ahmed Mohamed ameimarisha maudhui ya utabaka kwa kumchorea msomaji picha kuhusu ukwasi wa matajiri ambao unawapa mamlaka makubwa, kinyume na udhaifu wa watu maskini. Ukwasi wa Zuberi unadhihirishwa na vitu mbalimbali vya kifahari vilivyomo katika jumba lake.

7. Alikunja pazia la mlango, akapapasa ukuta wake na kuwasha swichi. **Taa zake za therea… zilimwitikia**… zikamwaya anga la kupendeza…(*Asali Chungu*, Ukur. 7)

Tashihisi ya taa za therea kumwitikia Zuberi inaashiria utabaka katika jamii ambapo kuna matajiri wenye uwezo wa kumiliki nyumba kama hii, kinyume na watu maskini ambao hawana uwezo huo. Lakini maelezo ya mwandishi kuhusu taa za therea hayalengi ujumi tu au kuusifu utajiri wa Zuberi. Mwandishi anasisitiza uwezo wa kiuchumi wa Zuberi kwa kumsisitiza mmiliki, yaani kwa kusema taa *zake zilimwitikia*. Mwandishi angesema tu, "akawasha taa." Maelezo ya mwandishi yanalenga kuchimuza kitendo cha kidhalimu cha Zuberi, tunayemwona akipita katika ukumbi wenye taa hizi za therea, akielekea kumbaka Semeni, msichana maskini mnyonge. Mamlaka aliyo nayo Zuberi yanamwezesha kutenda anavyotaka, bila kuhofia adhabu yoyote. Tashihisi iliyotumika inamfanya msomaji azingatie udhalimu huu.

Ishara nyingine ya mamlaka aliyo nayo Zuberi ni jumba lake. Jumba lake ni kubwa la kifahari, lenye kuta ndefu. Mwandishi amezirejelea kuta za jumba la Zuberi ili kusisitiza maudhui ya utabaka katika jamii, yaani tabaka la wenye nguvu za kiuchumi na tabaka la wale wasio na nguvu za kiuchumi. Matabaka hayo yanaashiria mahusiano ya kimamlaka kati ya matajiri na maskini. Kama tajiri na pia mfanyakazi wa ngazi ya juu serikalini, Zuberi anajihami ndani ya kuta ndefu.

8. Jumba hili lilikuwa lile lile. Kuta zake zilizokwenda juu ghorofa moja zilikuwa daima **zikiwakejeli** makafiri na wachochole. Waomba pesa wapitapo, husimama na kuinua nyuso zao kuangalia juu. (*Asali Chungu,* Ukur. 120)

Tashihisi "**kuta… zikiwakejeli makafiri…**" inaashiria nguvu za kiuchumi za mmiliki wa nyumba yenye kuta hizi. Kuta zinaukejeli unyonge wa maskini. Katika riwaya, tunaona jinsi ambavyo watu maskini hupita nje ya kuta hizi wakiombaomba. Maskini wanatambua tofauti kati ya uwezo wao mdogo wa kiuchumi na uwezo mkubwa wa matajiri kama Zuberi. Motifu ya pengo la kiuchumi baina ya matajiri na maskini imesisitizwa sana na mwandishi katika *Asali Chungu*.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi anaonyesha jinsi ambavyo raia walio wengi hawana uwezo wa kiuchumi wa kujipatia hata mahitaji ya kawaida ya maisha, kinyume na matajiri kama Zuberi na mke wake Amina. Matajiri wana uwezo wa kiuchumi wa kutosheleza mahitaji yao ya kawaida pamoja na kugharimia starehe yoyote wanayoitaka.

9. Mbali zile mboga na matunda ya viungo vya mchuzi; vyote vilikuwa **vikichekelea furaha na kuwaita wanunuzi** kujinunulia walichopenda. Kulikuwa na kila kitu sokoni kwa mwenye pesa zake, lakini kwa Dude palikuwa patupu. (*Asali Chungu,* Ukur. 78)

Katika dondoo la 9, tashihisi ya bidhaa kuwachekelea wanunuzi inachimuza ukosefu wa uwezo wa kiuchumi wa raia wengi. Mwandishi anaonyesha kweli kinzani iliyopo ambapo bidhaa zipo nyingi sokoni lakini wanunuzi hawana uwezo wa kiuchumi wa kuzinunua. Hiki ni kinaya. Tashihisi iliyotumika ya bidhaa kuwachekelea wanyonge lakini wasiweze kuzinunua pia inajenga tashtiti ambapo inaonekana kama kwamba mwandishi anaicheka hali hii. Tashtiti hii inadhihirisha na kusisitiza udhaifu wa kiuchumi wa raia wengi, kinyume na uwezo wa kifedha walio nao matajiri kama Amina na Zuberi.

Suala la umiliki wa ardhi nchini linafungamana na suala la mamlaka. Mwandishi anazungumzia hali ya kutokuwepo usawa katika umiliki wa ardhi nchini. Sehemu kubwa ya ardhi nchini inamilikiwa na makabaila wenye nguvu kubwa za kiuchumi, wakati ambapo raia wengi hawana ardhi.

10. 'Hili shamba lote ni la Bwana Zuberi. Huku halina mwisho, na huku mpaka bondeni. Halafu linapanda kilima; halafu linateremka, ndio **linapakana na Bi Amina**. Na **hilo lake linamwambia la Bwana Zuberi sogea huko**,' Bushiri alisema akiashiria. (*Asali Chungu,* Ukur. 92)

Akitumia tashihisi, mwandishi anaonyesha jinsi ambavyo makabaila wachache ndio wanaomiliki rasilimali muhimu ya ardhi. Ardhi ni msingi wa mamlaka. Matajiri wanautumia msingi huu kujiimarisha kiuchumi kwa njia ya ushuru mkubwa wanaoutoza wakulima maskini. Huu ni unyonyaji wa nguvu za maskini. Mwandishi ameuchimuza uwezo huu wa makabaila kwa njia ya tashihisi. Katika dondoo la 10 anaeleza kwamba shamba la Zuberi '…halina mwisho… linapakana na Bi Amina' badala ya kusema kwamba shamba hilo 'linapakana na *la* Bi Amina.' Kwa kutumia tashihisi, mwandishi analipa shamba uwezo wa kupakana na binadamu. Tashihisi hii inalenga kuchimuza uwezo wa Bi Amina unaotokana na umiliki wa shamba kubwa. Pia, mwandishi anatumia tashihisi: 'Na hilo lake [la Amina] linamwambia la Bwana Zuberi sogea huko.' Mwandishi anayapa mashamba ya Zuberi na Bi Amina uwezo wa kuzungumza pamoja. Katika kuhuisha mashamba ya makabaila hawa, mwandishi anatumia kiambishi *mw-* (katika 'lina*mw*ambia') kinachorejelea binadamu, badala ya kiambishi *li* (lina*li*ambia) ambacho kingerejelea shamba. Tashihisi hizi zinaashiria kwamba makabaila hawa wana ardhi kubwa inayozidi hata mahitaji yao, wakati ambapo maskini wanakabiliana na ukosefu wa ardhi.

### *Kinaya*

Mbinu ya kinaya vilevile imetumiwa na mwandishi wa *Asali Chungu* kuwasilisha maudhui ya mamlaka. Kwa mujibu wa Mbatiah (2001), kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile unachosema. Anasema kwamba kinaya kinatumiwa kutilia mkazo ujumbe fulani. Pia, huangaza utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo hasa. Inabidi msomaji autambue mwanya huo ili aweze kufahamu kile ambacho mwandishi anajaribu kuwasilisha katika kazi yake.

Saidi Ahmed Mohamed ametumia kinaya katika *Asali Chungu* kuimarisha maudhui ya utabaka. Anaonyesha kwamba hakuna usawa katika jamii anayoiandikia. Makabaila wamejitenga kitabaka na watu wa kawaida. Kinaya anachokitumia mwandishi kinahusisha matumizi ya neno 'waungwana.' Kwa mujibu wa TUKI (2013), 'muungwana' ni mtu "mwenye adabu na tabia zinazokubalika katika jamii."

11. Jikoni mfereji ulikuwa ukimwaya maji. Maji kila pahali – chooni, ambako **waungwana** wakikoga … (*Asali Chungu*, Ukur. 12)

Katika dondoo la 11 mwandishi anawarejelea Zuberi na mkewe Amina kama 'waungwana' kwa vile ni matajiri. Katika muktadha wa riwaya hii, hiki ni kinaya. Ni kinaya kwa sababu matajiri hawa kusema kweli sio waungwana. Hawana "adabu na tabia zinazokubalika katika jamii." Badala ya kuwa waungwana, matajiri wanaitumia nafasi yao kumnyonya mnyonge na kudumisha hali ya kutokuwepo usawa katika jamii. Kusudi la mwandishi ni kuihukumu hali hii kwa kuwasawiri Zuberi na mkewe Bi Amina kama watu wenye nguvu kubwa za kiuchumi, kinyume na raia wanaoishi katika umaskini mkubwa. Mwandishi analenga kumshawishi msomaji kuilaani hali hii.

Mwandishi analitumia neno 'waungwana' tena akiwarejelea Dude na Bi Amina, kutokana na uwezo wa kifedha wa Amina. Mwandishi ana sababu fulani ya kulitumia neno hilo tena kuwarejelea watu ambao kusema kweli sio waungwana.

12. Wote waliteremka. Mwenyeji wao, Mzee Mbaruku, mwangalizi wa nyumba ya Bi Amina, alifika hima kuwalaki; akawa anatoa mizigo waliyokuja nayo **waungwana**. (*Asali Chungu*, Ukur. 112)
13. Dau la kiasi lililetwa… Mzee Mbaruku akaanza kupakia mizigo kwenye hilo dau, na alipomaliza akawataka **waungwana** waingie. (*Asali Chungu*, Ukur. 114)

Mwandishi analirudia neno 'waungwana' mara mbili, akiwarejelea Dude na Bi Amina. Urudiaji huu unakusudia kujenga kinaya kwamba Amina na Dude kusema kweli, sio waungwana. Amina siye muungwana kwa sababu hana "adabu na tabia zinazokubalika katika jamii." Anamnyonya tu kijana maskini Dude ili kujistarehesha. Pia, mwandishi kumwita Dude 'muungwana' ni kinaya. Hii ni kwa sababu Dude ni kama mtumwa tu kwa Bi Amina. Dude hana mamlaka yoyote kwa sababu yeye ni maskini kabisa. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2013) 'dude' ni 'nyangarika' yaani kitu kisichokuwa na maana au thamani. Kwa kumwita 'muungwana,' mwandishi anauchimuza unyonge wa Dude wa kiuchumi kwa kuulinganua na uwezo mkubwa wa kiuchumi wa Amina.

Akitumia kinaya mwandishi wa *Asali Chungu* anaimarisha maudhui ya ukosefu wa nguvu za kiuchumi unaotokana na ukosefu wa ajira. Kwa upande mwingine matajiri wana nguvu kubwa za kiuchumi zinazotokana na nafasi zao serikalini.

14. Hawa, aliona Dude walikuwa wapagazi. Naye alikuwa **anawahusudu wapagazi** kila siku – vifua vyao vipana…walikuwa wanaume kweli kweli…

    (*Asali Chungu*, Ukur. 50)
15. Hapa lilimpita rikwama limepakia madondo; nyuma jengine limepakia nazi au mbata … Hilo pia litakuwa katika heka heka ya kupelekwa kwenye ghala ya tajiri mmoja. **Dude aliwahusudu wale wapagazi** waliokuwa wakitimka na yale marikwama… (*Asali Chungu*, Ukur. 75)

Sio sadfa mwandishi kurejelea mara mbili hali ambapo Dude anawahusudu wapagazi. Ingawa si jambo baya Dude kuwahusudu, mwandishi anachimuza ujumbe fulani kwa njia ya kinaya. Kinaya katika maelezo ya mwandishi kinajengeka katika muktadha kwamba hali ya wapagazi maskini siyo ya kuhusudika kwa kweli kwa sababu ni duni sana. Ni hali ya kukata tamaa. Wapagazi anaowahusudu Dude pia hawafaidiki sana na nguvu zao. Wanaofaidika ni matajiri wanaowaajiri wapagazi hawa. Mwandishi analenga kuimulika hali hii kwa kuonyesha jinsi ambavyo hali ya kiuchumi ya raia wa kawaida ni duni sana, wakati ambapo matajiri wanaendelea kujiimarisha kiuchumi kwa kumnyonya mnyonge.

Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana umepelekea ukosefu wa nguvu za kiuchumi. Vijana wengi wanashindwa kujikimu kimaisha. Mwandishi anatumia kinaya kuchimuza hali duni ya kiuchumi inayowakabili vijana. Vijana wamekata tamaa kabisa. Baadhi yao wanaona heri kufungwa gerezani ili angalau waweze kupata chakula.

16. …niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa na uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi hata kunipa chakula… Yakinijia mawazo hayo, huona nijitie katika hatia ili **nirudi jela ninusurike**. Hustahabu taabu ya kutumwa jela nikapata chochote, mradi silali na njaa… (*Asali Chungu,* Ukur. 83)

Vijana kama Bushiri hawana mamlaka yoyote ya kiuchumi. Ni wanyonge kiasi kwamba hawawezi hata kuhimili gharama ya chakula. Ni kinaya Bushiri kuiona jela kama mahali pa kumnusuru kutokana na hali ngumu ya kiuchumi nje ya jela. Hiki ni kinaya kwa sababu kufungwa jelani sio kunusurika bali ni kunyimwa uhuru. Mwandishi anailinganua hali hii ya kiuchumi inayowakumba vijina maskini na hali ya maisha ya matajiri kama Zuberi na Amina. Kinyume na vijana hawa, matajiri wana nguvu kubwa za kiuchumi zinazowawezesha kuhimili gharama zote za maisha.

**Hitimisho**

Makala haya yamechambua matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi katika kuibua maudhui ya mamlaka katika riwaya ya *Asali Chungu*. Tamathali hizi za usemi zinahusisha uchimuzi unaolenga ujumbe kwamba raia wengi katika jamii anayoiandikia mwandishi hawana mamlaka ya kiuchumi. Raia wachache ndio wana nguvu za kiuchumi. Hali hii inazalisha matabaka ya matajiri na maskini. Mahusiano kati ya matabaka haya mawili ni ya kiunyonyaji ambapo matajiri wananyonya jasho la mafukara wanyonge. Mahusiano haya pia ni ya kiudhalimu ambapo tajiri mwenye nguvu za kiuchumi anamwonea maskini bila kuhofia adhabu yoyote. Kupitia kwa tamathali za usemi, mwandishi anaikemea hali hii ya uonevu, unyonyaji pamoja na kuwepo kwa pengo kubwa kati ya raia wenye nguvu kubwa za kiuchumi na wale ambao ni wanyonge sana kiuchumi.

**Marejeleo**

Abrams, M. H. (1978). *A Glossary of Literary Terms.* Macmillan India Limited.
Dahl, R. A. (1957). *The Concept of Power.* Yale University
Fairclough, N. (1996). *Language and Power.* Addison Wesley Longman Limited.
Kazungu, K. (1982). Deviation and foregrounding in chosen literary texts [Unpublished master's thesis]. University of Nairobi.
Kipacha, A. & Jilala, H. (2021). *Nadharia za Elimumitindo ya Kiswahili.* Daud Publishing Company Ltd.
Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Standard Textbooks, Graphics and Publishing.
Meniailo, V. (2020). V. Arnold's Theory of Foregounding and its Application to Text Analysis. *Interliteraria*, 25/1:1 16 – 25.
Mohamed, S.A. (1978) *Asali Chungu*. East African Educational Publishers.

Murithi, J. J. (2017). Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. [Unpublished doctoral dissertation]. University of Kenyatta.

Osoro, G. (2003). Uhakiki wa riwaya za Said Ahmed Mohamed. [Unpublished master's Dissertation]. University of Nairobi.

Thomas, L. na wenzake (2004). *Language, Society and Power.* Routledge.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. TUKI.

Van Peer, W. & Hakemulder, J (2006). Foregrounding. *Encyclopedia of Language and Linguistics, 4,* 546-550.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Focus Publications Ltd.